

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
7 Machi 2009**

**Waliohudhuria**

Bashiri Rashidi  
Dominata Rwechungura  
Edgar R Paulo  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Hamadi Hatibu Bwaja  
Husein Hamza Hamisi  
Juma Ali Salehe Jongo  
Mohammed Samwely  
Paulo Atibu Hatibu  
Shamte J Kigoma  
Sudi Saidi Ramadhan

**Mradi wa Wamba**

Mohammed alitoa repoti kuhusu mafunzo ya usalama wa baisikeli shule ya Kigamboni ya jumamosi mbili zilizopita, na walimu walikuwa Mohammed Samwely, Ali Saidi Mwishehe, Paulo Atibu, Dominata Rwechunguru na Mwalimu Emmanuel. Mafunzo yalienda vizuri na taarifa zaidi zipo ndani ya repoti yake. Wanafunzi 47 walishiriki wiki ya kwanza lakini 37 tu walishiriki wiki ya pili – wasichana 8 na wavulana 29 kutoka miaka 14 mpaka miaka 19. Mama Wamba alikuwa mgeni rasmi kwa ajili ya kutoa vyeti mwishoni. Elaine atachapa repoti Mohammed aliyandika.

Mohammed alisanya kurasa za mahudhurio. Ali Saidi Mwishehe ana fomu za maswali lakini hakuwepo leo. Resiti zote bila hiyo ya kuprint kwenye jaketi zililetwa kwa Juma. Filbert, Hamadi na Ali Saidi Mwishehe walipewa Tsh 485,000 na walitumia Tsh 469,700 na walirudisha Tsh 15,300. Mohammed alipewa Tsh 230,000, alitumia Tsh 200,000 na alirudisha Tsh 30,000. Mohammed pia aliandika repoti ya matumizi.

Tuliprint nembo na jina la UWABA kwenye jaketi za reflecta na zimependeza. Ali Saidi Mwishehe ana jaketi na helmeti zilizobaki.

Una Osili wa Wamba Memorial Fund alimwandikia email Elaine na taarifa zaidi kuhusu transfer ya hela alitumia. Edgar atafuatalia na benki wiki hii.

**Ruzuku ya Foundation for Civil Society Grant**

Elaine aliandika maombi. Wanachama walipitisha na walisahihisha. Tumekosa tarehe ya kwanza Machi basi itabidi tupeleke tarehe 1 Julai. Elaine atapata CV za waalimu wa kompyuta kuweka pamoja na maombi.

**Mkutano na serekali ya jiji na kongamano**

Elaine aliwasiliana na Bwana Japhet kwa simu. Alisema wiki ijayo itakuwa nzuri kwa mkutano lakini atawasiliana jumatatu kutuambia tarehe. Elaine atawajulisha wanachama wengine na message ya simu.

### **Baiskeli kutoka kwa Re-cycle**

Elaine bado hajakata jibu kutoka Andrew ya ushauri kuhusu kuchagua watu kuwapa baiskeli.

### **Juma**

Kwa sababu ya matatizo ya familia Juma alihamia ofisi ya UWABA. Wanachama walisema watakubali alale pale kama kuna haja lakini atoe vitu binafsi vyake ili ionekani kama ofisi ya kweli. Juma alikubali.

### **Mambo ya hela na guta**

Filbert alileta Tsh 21,000 ya hela ya guta na bado anadaiwa Tsh 7,000. Hela ambayo inabaki kutoka mafunzo ya Wamba ni Tsh 45,300. Tulilipa posho ya Juma ya mwezi wa pili Tsh 20,000. Tulirudisha mkopo ya Shukuru Tsh 7,000. Edgar ataweka hela ya Tsh 40,000 ndani ya akaunti ya benki wiki hii.